



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

UCHAGUZI MDOGO KWENYE KATA TATU

Dar es Salaam, 13 Novemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuutaarifu umma kwamba imeandaa uchaguzi mdogo kwenye kata tatu ambazo kutokana na sababu mbalimbali hazikuweza kufanya uchaguzi tarehe 28 Oktoba 2020 ambayo ilikuwa siku ya Uchaguzi Mkuu. Kata hizo ni:-

- Nyahanga, iliyopo kwenye Halmashauri ya Mji wa Kahama, Mkoani Shinyanga,
- Igumbilo, iliyopo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Mkoani Iringa,
- Kibosho Kati, iliyopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa kifungu cha 51(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kikisomwa pamoja na kanuni ya 33 ya kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, Tume imepanga tarehe 16 Novemba, 2020 kuwa ni tarehe ya uteuzi wa wagombea wa vyama ambavyo wagombea wake walifariki kwenye kata ya Nyahanga na Igumbilo.

Kampeni za uchaguzi kwenye kata tajwa zitafanyika kwa siku 21 kuanzia tarehe 17 Novemba, 2020 hadi 07 Desemba, 2020 na uchaguzi utafanyika tarehe 8 Desemba, 2020.


Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 48(1) (b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tume imepanga tarehe 8 Desemba 2020 kuwa siku ya uchaguzi kwa Kata ya

Kibosho Kati, ambayo haikufanya uchaguzi wa Diwani kutokana na kukosewa kwa karatasi za kura za Kata hiyo.

Ni vyema ikafahamika kwamba kwenye Kata hiyo ya Kibosho Kati hakutakuwa na kampeni kwa kuwa kampeni zilishafanyika. Hivyo basi, wapiga kura wa Kata hiyo wanaombwa kujitokeza kwa wingi siku hiyo ya uchaguzi ili kumchagua diwani wanayemtaka.

Tume inachukua fursa hii kuwakumbusha watendaji wa uchaguzi kwenye kata hizo kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume. Vilevile, Tume inavikumbusha vyama vya siasa na wagombea kuhakikisha wanafuata utaratibu wa kisheria kuweka mawakala kwenye vituo vyote vya kupigia kura ili kuhakikisha kwamba maslahi ya wagombea yanalindwa.

Aidha, vyama vya siasa na wagombea wanakumbushwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 na kuwahimiza wanachama na wafuasi wao kudumisha amani kipindi chote cha kampeni na siku ya uchaguzi.



Gerald G. J. Mwanilwa

KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI